



## Dunia ni starehe, na starehe yake bora ni mke mwema

Imepokewa kutoka kwa Abdallah Ibn Amri -Radhi za Allah ziwe juu yao wawili-  
yakwamba Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Dunia ni starehe, na  
starehe yake bora ni mke mwema".

[Sahih] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa Dunia na vyote vilivyomo si kingine isipokuwa ni kitu cha kustarehe nacho kwa muda mchache kisha kinaondoka, nakuwa starehe yake bora ni mke mwema, ambaye akimtazama anamfurahisha, na akimuamrisha anamtii, na akiwa mbali naye humuhifadhi ndani ya nafsi yake na mali yake.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/5794>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

